














Nuhu na Mafuriko ya ajabu

Hadithi kutoka kwa Neno la Mungu, Bibilia,

inapatikana katika

Mwanzo 6-10

“Kufafanusha maneno yako kwatia nuru.”
Zaburi 119:130

Kimeandikwa na Edward Hughes
Kimeorodheshwa na Byron Unger; Lazarus

Kimetafsiriwa na Grace Chepkoech
Imerekebishwa na M. Maillot; Tammy S.

Hadithi 3 baadhi ya 60

**M1914.org**

**Bible for Children, PO Box 3, Winnipeg MB R3C 2G1 Canada**

Leseni: Unahaki ya kunakili au kuchapisha hadithi hii. Mradi tu.

**Mungu anajua** kuwa tumetenda mambo mabaya, anayoyaita dhambi. Mshahara wa dhambi ni mauti.

**Mungu anatupenda** sana hadi akamtuma mwana wake, Yesu, aje afe msalabani na alipe mshahara ule wa dhambi. **Yesu alifufuka** na akarudi mbinguni! Sasa Mungu anaweza kusamehe dhambi zetu.

**Kama unataka kuondoka kwa dhambi zako,** mwambie Mungu haya: Mungu mpendwa, ninaamini kuwa Yesu alikufa kwa ajili yangu na anishi tena. Tafadhali njoo maishani mwangu na usamehe dhambi zangu, ili niwe na maisha mapya na niwe nawe milele. Nisaidie niishi kwako kama mtoto wako. Yohana 3:16

**Soma bibilia na zungumza na Mungu kila siku!**

Kiswahili Swahili







Mungu alimpa ilani Nuhu kuwa mafuriko makuu yatatokea na kufunika ardhi yote. “Jenga safina,” machela kubwa inayotosha familia yake na wanyama wengi. Nuhu aliamrishwa. Mungu alimwuelezea kila atakacho fanya. Sasa Nuhu akaanza kazi!
3
Watu walimchekelea Nuhu alipojaribu kuwaelezea sababu yake ya kujenga safina. Hata hivyo, Nuhu aliendelea kujenga. Pia alizidi kuwaelezea kumhusu mungu. Hakuna aliyemsikiliza.
4
Nuhu alikuwa na imani kubwa. Almwuamini Mungu hata kama mvua haikuwa imewahi kunyesha hapo mbeleni. Baadaye safina ilikuwa tayari.
5
Sasa, wanyama wakaja. Mungu aliwaleta aina saba ya wanyama na wawili wa wengine.
6
Ndege wakubwa kwa wadogo, wanyama warefu kwa wafupi wakaingia ndani ya safina.
7
Pengine watu walimtukana Nuhu alipokuwa akiwaingiza wanyama. Waliendelea kutenda dhambi. Hawakutaka kuingia ndani ya safina.
8
Mwishowe, wanyama wote na ndege wakawa ndani. “Njoo ndani ya safina,” Mungu akamualika Nuhu.
9
“Wewe na familia yako.” Nuhu, bibi yake, wana wake watatu na bibi zao wakaingia ndani ya safina. Hapo Mungu akaufunga mlango wa safina!
10
Mvua mkubwa ukaanza kunyesha. Kulinyesha kwa muda wa siku arobaini.
11
Maji yalifurika na kufunika miji na vijiji.
12
Wakati mvua uliisha, hata milima ilikuwa imefunikwa. Kila kitu chenye uhai kilikufa.
13
Mafuriko yalipozidi nayo safina iliendelea kuelea juu ya maji. Labda kulikuwa na giza ndani, labda hakukuwa na starehe au hata kulikuwa kunatisha ndani ya safina. Lakini safina iliwapa Nuhu na jamii yake usalama.
14
Baada ya miezi mitano ya mafuriko, Mungu alituma upepo wa kukausha maji. Kwa muda, safina ikaja kutulia juu ya milima ya Ararat.
15
Nuhu walikaa ndani ya safina kwa muda wa siku arobaini maji ilipozidi kupungua.
16
Nuhu akamtuma kunguru na njiwa nje ya safina kupitia dirisha. Alipokosa mahali pa kutua, njiwa akarudi.
17
Baada ya wiki, Nuhu akajaribu tena. Wakati huu njiwa alirudi na jani bichi la mzeituni kinywani mwake. Siku iliyofuata Nuhu akajua kuwa ardhi ilikuwa imekauka kwa vile njiwa hakumrudia.
18